# HALMASHAURI YA MJI KONDOA

## HABARI ZA WIKI

TOLEO NA:3

JUMATATU, FEB 06-FEB 12, 2023


BARAZA LA BAJETI




## BARAZA LA MADIWANI KONDOA MJI LAPITISHA BAJETI YA 2023/2024 YENYE ONGEZEKO LA SHILINGI MILIONI 248.9

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Mji Kondoa limepitisha rasimu ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 wenye ongezeko la shilingi milioni 248.9 kutoka fedha za mapato ya ndani ikilinganishwa na bajeti inayoendelea kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Rasimu hiyo ilisomwa na Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Halmashauri ya Mji Kondoa, Thecla Nyoni kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wakati wa mkutano maalum cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri hivi karibuni.

Aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Mji wa Kondoa imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi 20,161,963,000.00 ikiwa ni ziada ya shilingi 248,985,000.00 sawa na asilimia 1.2 ya bajeti ya mwaka 2022/2023. Aidha, bajeti ya mapato ya ndani imeongezeka kutoka shilingi 1,659,900,000.00 mwaka 2022/2023 hadi shilingi 1,908,885,000.00 mwaka 2023/2024 ikiwa na ongezeka la asilimia 13.

YALIYOMO NDANI


“MAFUNZO YA UTAWALA BORA YAKABORESHE UTENDAJI WETU” – DKT. ASHATU
UK. 3

MADIWANI WATAKIWA KUSHIRIKIANA KULETA MAENDELEO KONDOA
UK. 4

MWENYEKITI ATOA MASUFURIA SHULENI KUUNGA MKONO JUHUDI ZA WAZAZI
UK. 5

TAKUKURU RAFIKI KUIMARISHA UTAWALA BORA KONDOA
UK.6

WAKULIMA WASHAURIWA KUTUMIA VIATILIFU VYENYE UBORA
UK.7

# BARAZA LA BAJETI



INATOKA UK 1

## BARAZA LA MADIWANI KONDOA MJI LAPITISHA BAJETI YA 2023/2024 YENYE ONGEZEKO LA SHILINGI MILIONI 248.9

Bajeti ya mwaka 2023/2024 imeongezeka kutokana na kuongeza viwango vya ukusanyaji kwa baadhi ya vyanzo pamoja na kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato.


Alivitaja vyanzo vipya vitakavyoanza kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/24 kuwa ni kuanza kukusanya ushuru wa maegesho ya magari, ushuru wa huduma kutoka kwa wakandarasi wanaofanya kazi za ujenzi kupitia TARURA, TANROADS, REA na RUWASA. Vingine ni mapato ya mitaa na kata kuwa kuwa sehemu ya bajeti za Halmashauri kutokana na kuanza kutumia mfumo wa FFARS ngazi ya mitaa na kata.

Alisema kuwa Halmashauri ya Mji Kondoa pia katika maandalizi hayo ya rasimu ya bajeti imezingatia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Mwongozo wa bajeti 2023/2024 vikielekeza kugawa fedha za mapato ya ndani halisi asilimia 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na asilimia 80 kwa ajili ya uendeshaji wa Halmashauri.

Awali akiwasilisha rasimu hiyo Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri ya Mji Kondoa iliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi 19,912,978,000.00 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za maendeleo ambapo hadi kufikia Desemba, 2022 kiasi cha shilingi 8,557,362,349.82 sawa na asilimia 43 ya fedha idhinishwa kimepokelewa.

Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/2024 umezingatia tathmini ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Mapitio ya Utekelezaji wa nusu mwaka wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo mafanikio yamebainishwa na changamoto zilizojitokeza zimewekewa mikakati ya kuondolewa au kupunguzwa katika Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.








## MAFUNZO UTAWALA BORA



## "MAFUNZO YA UTAWALA BORA YAKABORESHE UTENDAJI WETU" – DKT. ASHATU

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amewashauri waheshimiwa Madiwani na kuwataka watendaji wote wa kata, mitaa na vijiji Wilaya ya Kondoa kuzingatia mafunzo ya utawala bora watakayopewa kwa siku mbili kwa ajili ya kuboresha utendaji wao wa kazi.

Kauli hiyo aliitoa wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo yanayotolewa na shirika lisilo la kiserikali la CETA kwa ufadhili wa shirika la kijerumani la Hanns Seidel Foundation uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Kondoa Irangi hivi karibuni.

"Mhe. Rais amesema lazima viongozi wote wapewe elimu ya wanachoenda kutekeleza na hapa ndio tupo tumeanza kutekeleza kwa vitendo, kwa kuwa elimu ni jambo la msingi katika kila kitu unachofanya," alisema Dkt. Ashatu.

Aliongeza kwa kusema kuwa shirika la Hanns linafanya kazi nzuri na wamekuwa wakifanya katika maeneo mengine hivyo, amewakaribisha katika Wilaya ya Kondoa na kuwataka wakurugenzi, wakuu wa idara na watendaji wote kusikiliza kwa umakini na kuelewa kwa pamoja maana ya utawala bora.

"Inawezekana mnatekeleza wajibu na majukumu yenu vizuri ila hamzingatii sheria zilizopo. Hivyo, nina imani wenzetu watatuambia wajibu wetu na majukumu yetu kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kujua namna ya kuwafikishia maendeleo wananchi," alisema Mhe. Ashatu.

Aidha, aliwashauri wakufunzi wa CETA kuwaambia waheshimiwa madiwani walioaminiwa na wananchi baada ya kuomba nafasi za uongozi jinsi ya kwenda na wananchi ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuwashirikisha ili kujua vipaumbele vyao.

Akiongea awali mwakilishi wa shirika la Hanns, Kadele Mabumba alisema shirika hilo linafanya kazi ya kuwajengea uwezo viongozi wa serikali ili waweze kusimamia majukumu yao na hiyo si mara ya kwanza kwani wamekuwa akifanya hivyo kwa vipindi tofauti.

"Kwa kweli toka tumeanza kutoa mafunzo tumeona mabadiliko maeneo tuliyopita ambapo kwasasa uwazi na upangaji wa matumizi ya fedha za srikali umeongozeka, mapato ya ndani yameongezeka, yameongeza ushiriki wa wananchi katika mikutano yao na kupunguza migogoro katika jamii" alisema Kadele.

Uzinduzi huo ulifanyika kwa kuhudhuriwa na viongozi wa Chama cha Mapinduzi, Kamati ya Usalama, waheshimiwa Madiwani, wakurugenzi, wakuu wa Idara, maafisa Tarafa, watendaji wa Kata na Mitaa wote wa Wilaya ya Kondoa ambapo mafunzo yatatolewa kwa viongozi zaidi ya 300 katika kata zote 29 na vijiji 84

## BARAZA ROBO YA PILI



## MADIWANI WATAKIWA KUSHIRIKIANA KULETA MAENDELEO KONDOA

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Waheshimiwa madiwani wametakiwa kuongeza umoja na ushikamano uliopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuwa wameaminiwa na wananchi na wameibeba dhamana ya Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoa Mhe. Mohamed Kiberenge wakati akiongea katika mkutano wa Baraza la Madiwani la robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji Kondoa.

“Tushirikiane kwa pamoja mafanikio ya mji yanataka umoja siyo kubezana au kuona jambo la mtu mmoja si kweli lazima kila mmoja anayejihisi ni mdau katika Mji huu wa Kondoa naye aoneshe amesaidia nini katika jambo moja au rasilimali,” alisema Mhe. Kiberenge.

Aidha, alisema kwa upande wa elimu sekondari katika matokeo ya kidato cha Nne Halmashauri haijafanya vizuri. Hivyo, wamemtaka Afisa Elimu Sekondari kufanya tathmini ya sababu zilizopelekea kushuka kwa ufaulu kwa kidato cha Nne na Pili japokuwa kuna baadhi ya shule ufaulu umepanda.

“Ukaangalie shida ni mwalimu mmoja mmoja wa somo, shida ni walimu au ushirikishwaji wa walimu si mzuri au hawataki kuwajibika au mwalimu alikuwa na shida gani lazima tujue kata nane tulitakiwa kuwa nafasi nzuri madiwani wapate taarifa na chama ili ufanyike ufuatiliaji wa pamoja,” alisisitiza Mhe. Kiberenge.

Aliongeza kwa kuzitaka kamati za mazingira kusimamia suala la utupaji hovyo wa taka na kuona ni jambo la pamoja na si la mtu mmoja. Hivyo, waheshimiwa madiwani wakakae na kamati za kata ili kuweka mkakati wa pamoja na kufanya doria za mara kwa mara za kukagua usafi wa mji, aliongeza.

Kwa upande wa afya aliwataka madaktari na wauguzi kuwajibika kwa nafasi zao kwa kutoa huduma kwa wananchi kwa kutumia lugha nzuri ili wananchi wafurahie huduma wanazopatiwa na kuokoa uchumi wao hasa wanaoenda Dodoma kupatiwa huduma.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kondoa, Mhe. Hija Sulu aliwataka waheshimiwa madiwani kwenda kuwaelezea wananchi mafanikio kwenye kata zao na kuwataka kushirikiana, kupendana na kuvumiliana kama familia moja kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi.

## ELIMU SEKONDARI



## MWENYEKITI ATOA MASUFURIA SHULENI KUUNGA MKONO JUHUDI ZA WAZAZI

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoa, Mhe. Mohamed Kiberenge ametoa masufuria manne makubwa katika shule mbili za sekondari ikiwa ni kuunga mkono jitihada za wazazi za kutoa chakula shuleni.

Makabidhiano hayo yalifanyika katika shule za Tura Day Sekondari na Ula Sekondari na kupokelewa na wakuu wa shule hizo hivi karibuni.

“Natimiza ahadi niliyoitoa kwenye vikao vya wazazi wa shule hizi ili kuhakikisha tunapata mafanikio ya elimu niliahidi kutoa sufuria na leo nakabidhi ikiwa ni wiki mbili tu zimepita toka niahidi” alisema Mhe. Kiberenge.

Aliongeza kuwa anathamini nguvu za wazazi za kuhakikisha elimu inasimama kwa kuwa ni yao pamoja na kuwasihi wazazi kuwa karibu na shule na kushirikiana na walimu ikiwa ni pamoja na kuchangia nguvu zao ili kuhakikisha elimu inasonga mbele.

“Natoa wito kwa wazazi kuwa elimu ni haki ya mtoto msiwanyanyapae na kuwakatia tamaa wototo wenu. Msione hawana akili, wanazo nyingi tu ila muwe nao karibu na kuwaunga mkono watafanya vizuri tu” alisisitiza Mhe. Kiberenge.

Aidha, alitoa masufuria manne yenye thamani ya shilingi 280,000, ambapo matatu yameenda katika shule ya Sekondari Ula na moja shule ya Sekondari Tura Day na lengo ni kuunga juhudi jitihada za wazazi kwenye elimu na anatarajia kuanza ziara ya kuongea na wazazi wa mitaa mingine ili washiriki kwenye masuala ya elimu.





## BARAZA ROBO YA PILI



## TAKUKURU RAFIKI KUIMARISHA UTAWALA BORA KONDOA

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Serikali imeanzisha program mpya iitwayo TAKUKURU RAFIKI yenye lengo la kuimarisha utawala bora kuanzia ngazi ya chini hadi juu kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi.

Utambulisho wa program hiyo ulifanywa na Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Kondoa, Michael Sanga wakati wa Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji Kondoa hivi karibuni.

"Program hii itafanya kazi sehemu zote ikiwemo usimamizi wa miradi ambapo kitafanyika kikao katika ngazi ya kata na mitaa na Mheshimiwa Diwani atakuwa Mwenyekiti. Katika kikao hicho zitaibuliwa kero na wataalam watajibu, kero ambazo zitakosa majibu zitachukuliwa na TAKUKURU hadi ngazi ya Wilaya kwa mtaalam husika kutafuta ufumbuzi," alisema Kamanda Sanga.

Aliongeza kwa kusema kuwa katika vikao hivyo, yatawekwa maazimio na kupewa muda wa utekelezaji na TAKUKURU watafuatilia utekelezaji wake na lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha si kila kero inafika ngazi za juu wakati inaweza kutatuliwa kwa ngazi husika.

"Wanaotoa huduma wanatakiwa kuwajibika kwa nafasi zao kwa majukumu yao na wanaopokea huduma. Vilevile, wanapaswa wapate huduma wanayoitarajia katika ngazi husika na lengo ni moja tu kuhakikisha wananchi wanapata huduma" alisema Kamanda Sanga.

Program ya TAKUKURU RAFIKI itasimamiwa na Ofisi ya TAKUKURU na katika vikao vya ngazi ya chini itaongozwa na Diwani wa kata husika kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji lengo likiwa ni kuimarisha utawala bora kwa ngazi zote.





## KILIMO



# WAKULIMA WASHAURIWA KUTUMIA VIATILIFU VYENYE UBORA

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Wakulima wa Kata ya Serya wameshauriwa kutumia viatilifu vyenye ubora na vinavyoshauriwa na wataalam wa kilimo kwa ajili ya kudhibiti viwavi jeshi vamizi ili wapate mavuno mazuri.

Ushauri huo ulitolewa na Afisa Ugani wa Kata ya Serya, Melczedeck Nyigo alipowatembelea wakulima wa kata yake kwaajili ya kuwashauri masuala mbalimbali ya kitaalam ya kilimo ili wawe na mavuno mazuri na kuwa na uhakika wa chakula.

"Nawashauri pia mzingatie kufanya palizi kwa wakati ili mahindi yasiharibikie shambani maana majani yakuvamia shamba utavuna mahindi kidogo kwa kuwa yatakosa sehemu ya kuchanua maana yatazongwa na majani tutarudi kwenye njaa" alisema Nyigo.

Aidha, aliwataka kuhakikisha viatilifu wanavyotumia kuvinunua katika maduka yanayotambulika ili kuepuka kununua viatilifu vitakavyoharibu mazao yao na kushindwa kuwatambua waliowauzia.

Afisa Ugani huyo alitoa elimu hiyo kwa mkulima mmoja mmoja kwa lengo la kuhakikisha wakulima katika eneo lake wanalima kisasa kwa kutumia eneo dogo na wanapata mavuno mengi hali ambayo itawahakikishia uwepo wa chakula hapo baadae.





# TAARIFA MBALIMBALI/MATANGAZO YA IDARA

## SALAAM ZA PONGEZI KWA MHESHIMIWA MBUNGE

BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI NA MENEJIMENTI WANAMPONGEZA MBUNGE WA KONDOA MJINI MHE. JUMA ALLY MAKOA KUCHAGULIWA KUWA MWENYEKITI WA KAMATI YAHAKI,MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE NA MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA UTALII KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.



## TANGAZO LA KUONESHWA MAENEO YA KUJENGA VIBANDA STENDI YA MABASI BICHA


MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWATANGAZIA WAFANYABIASHARA WOTE WALIOLIPIA FOMU KWA AJILI YA VIBANDA KATIKA STENDI MPYA YA MABASI BICHA KUFIKA KATIKA STENDI HIYO SIKU YA IJUMAA YA TAREHE 17/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI KWA AJILI YA KUONESHWA SEHEMU ZA KUJENGA VIBANDA.
AIDHA BAADA YA KUONESHWA MAENEO HAYO WAFANYABIASHARA HAO WATAPASWA KUSAINI MIKATABA KABLA YA KUANZA UJENZI WA VIBANDA.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

## Kuelekea siku ya Wanawake Duniani Machi 8,2023

WANAWAKE WOTE WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA MNAKUMBUKUSHWA KUWA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI KIMKOA ITAADHIMISHWA KATIKA WILAYA YA KONDOA TAREHE 8/03/2023. SARE ZA SIKU HIYO ZINAPATIKANA KATIKA OFISI YA MAENDELEO YA JAMII HALMASHAURI YA MJI KONDOA KWA BEI YA SHS. 24,000/=TU AU PIGA SIMU NAMBA 0717635848.

KARIBUNI SANA



KAULI MBIU:*"UBUNIFU NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA,HACHU KATIKA KULETA USAWA WA KIJINSIA"*

# PICHA MBALIMBALI KATIKA BARAZA LA ROBO YA PILI 2022/2023









## MIRADI ILIYOTEMBELEWA NA MKURUGENZI KUFUATILIA UTEKELEZAJI WAKE





UJENZI WA KITUO CHA AFYA KOLO





UJENZI WA WODI HOSPITALI YA MJI